# Unapotaka kufuga samaki kambale

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. Na. 15, Jumatano Februari 5, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100

## KUMALIZA MZOZO WA DRC...

# Dk. Samia awaleta Kagame, Tshisekedi Dar

"Kwa mujibu wa Rais William Ruto wa Kenya ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mkutano huo utafanyika Ijumaa na Jumamosi wiki hii jijini Dar es Salaam na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekubali kupokea ugeni utakaokuja.

- WAJA KUJADILI, KUFIKIA SULUHU LA VITA VINAVYOENDELEA GOMA NDANI YA DRC
- UTAWAKUTANISHA PIA MARAIS KUTOKA AFRIKA KUSINI, KENYA, SOMALIA, UGANDA, ZIMBABWE
- MKUTANO UNAFANYIKA WAKATI UN IKISEMA WATU 900 WAMEUAWA NA WENGINE 2,880





KAGAME



TSHISEKEDI

# Kanuni za kufanikiwa kimaisha

# Watendaji ardhi waonywa

NA MWANDISHI WETU

**SERIKALI imewataka watendaji wa Sekta ya Ardhi nchini kutochelewesha huduma za sekta ya Ardhi kwa makusudi wakati wanapowahudumia wananchi wanaokwenda kupata huduma katika ofisi zao.**

Hayo yameelezwa hivi karibuni mkoani Iringa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansoor wakati wa kikao kazi cha watumishi wa Sekta ya Ardhi Mkoa wa Iringa.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mhandisi Anthony Sanga, Mansoor amesema kumekuwa na ucheleweshaji huduma kwa makusudi na wakati mwingine watendaji wa sekta ya Ardhi kuwatuma mwananchi wanaokwenda kupata huduma.

Aidha, Mansoor kupitia kikao hicho kilichoandaliwa na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa ametaka kuwekwa utaratibu rasmi katika ofisi zote za Ardhi kuanzia ngazi ya wilaya wa namna ya kupata hati ili wananchi wauelewe na kuufuata utaratibu huo.

Kwa upande wake Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa Frank Minzikuntwe ameeleza kuwa, kikao kilichofanyika cha watumishi kilikuwa na lengo la kuzungumza na kupeana mikakati pamoja na mipango kazi ya namna ya kushughulikia kero na utoaji huduma za sekta ya ardhi kwa haraka zaidi.

Kikao hicho cha siku moja kimeshirikisha watendaji wa sekta ya ardhi kutoka halmashauri zote za mkoa wa Iringa pamoja na wale wa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Iringa.

# Wajengewa uwezo miradi ya upimaji

NA MWANDISHI WETU

**WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI) imeendesha semina ya kuwajengea uwezo wadau wa mradi huo kutoka taasisi mbalimbali kuhusiana na namna mradi mradi huo unavyorahisisha kazi katika maeneo yao.**

Semina hiyo imefanyika hivi karibuni katika Kituo cha Ubunifu na Mafunzo ya Kijiografia kilichopo eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) jijini Dodoma ambayo imehusisha wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za serikali zinazotegemea na kutumia taarifa za kijiografia kutekeleza majukumu yao.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga, Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Hamdouny Mansoor amesema semina hiyo inalenga kuwajengea uwelewa zaidi wataalamu hao kuhusu mradi wa LDI ili kuimarisha uhusiano mzuri uliopo miongoni mwa taasisi za Serikali hatua itakayosaidia kutekeleza mradi huo kwa pamoja kwa ufanisi zaidi.

"Kutokana na umuhimu wa taasisi, tumeandaa semina hii ili kuwajengea uwelewa zaidi kuhusu mradi tukiamini hatua hii itaongeza uhusiano mzuri uliopo na taasisi na kwa pamoja kutekeleza mradi kwa ufanisi," alisema Mansoor.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mkurugenzi huyo wa Upimaji na Ramani ameongeza kuwa mradi huo wa LDI unaboresha miundombinu ya upimaji inayoleta taarifa zote za ardhi katika ukamilishaji wake.

Amesema, lengo kubwa la mradi huo wenye thamani ya dola milioni 65 unafadhiliwa na serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini utasaidia kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima pamoja na kuboresha teknolojia ya upimaji.

"Mradi huu una umuhimu wa kipekee katika sekta nyingine zinazotegemea taarifa za kijiografia katika kutekeleza majukumu yake na mfano ni katika miradi mikubwa ya kimkakati ya ujenzi wa miundombinu, utunzaji mazingira, utalii na udhibiti wa maliasili pamoja na ulinzi wa usalama wa nchi," alisema Mansoor.

Mradi huo ni uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali ili kuboresha huduma upatikanaji huduma na taarifa sahihi za kijiografia kwa wakati zikiwemo ramani za msingi ambazo ni nyenzo muhimu katika utawala wa ardhi hususan kupanga, kupima na kumilikisha.

# Kanda ya Songea wapata elimu ya sheria

NA ALBANO MIDELO

**WANANCHI zaidi ya 2,206,169 kutoka Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mtwara, na Lindi wamepata elimu ya sheria kupitia mabanda yaliyokuwa katika Soko Kuu Songea na vipindi vya redio za kijamii.**

Hayo yamesemwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Songea James Karayemaha wakati anazungumza katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria nchini iliyoanza 25 Januari 25,2025 na kufikia tamati Februari Mosi 2025.

Jaji Karayemaha amesema Wiki ya sheria imelenga kupunguza hofu dhidi ya mfumo wa mahakama, majaji, mahakimu, polisi, na taasisi za kupambana na rushwa.

Maadhimisho ya mwaka huu yanaongozwa na kauli mbiu:

"TANZANIA YA 2050: Nafasi ya Taasisi Zinazosimamia Haki Madai Katika Kufikia Malengo Makuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo."

Jaji Mfawidhi amesisitiza umuhimu wa misingi ya haki na amani katika maendeleo ya taifa. Pia, amezitaka taasisi za haki madai kushirikiana kwa karibu kuhakikisha mfumo wa sheria unachangia kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

Wadau waliotoa mchango mkubwa katika wiki ya sheria ni pamoja na Jeshi la Magereza, Polisi, Mawakili wa Serikali, TLS, TAKUKURU, Zimamoto, Uhamiaji, Vodacom, NMB, NBC, na taasisi nyingine nyingi.



# Dk. Samia awaleta Kagame, Tshisekedi Dar

NA CHARLES MATESO

**WAKATI waasi wa M23 wakitangaza kusitisha mapigano Mashariki wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa kile walichodai 'kwa sababu za kibinadamu', Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa wiki atakuwa mwenyeji katika ugeni mzito utakaojadili hali halisi ya vita nchini humo.**

Waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda lilitaja 'sababu za kibinadamu' ndizo zinazokwenda kusitisha mapigano, baada ya kuteka maeneo kadhaa ya mashariki mwa nchi hiyo.

Kwa mujibu wa Rais William Ruto wa Kenya ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mkutano huo utafanyika Ijumaa na Jumamosi wiki hii jijini Dar es Salaam na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekubali kupokea ugeni utakaokuja.

Mkutano huu unafanyika kufuatia makubaliano kati ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ambaye ni Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa pamoja na Rais Ruto.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekubali kuwa mwenyeji wa mkutano uliokusudiwa kufanyika kujadili hali ilivyo Mashariki mwa DRC," alisema Rais Ruto.

Kwa mujibu wa Rais Ruto, Rais Felix Tshisekedi wa DRC na Rais Paul Kagame wa Rwanda wamethibitisha kuhudhuria mkutano huo, ambao utatanguliwa na kikao cha mawaziri siku ya Ijumaa kabla ya wakuu hao kukutana Jumamosi.

Rais Ruto alithibitisha, kufanikisha mkutano huo mbali na jitihada za Dkt. Samia pia aliwashirikisha Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini, Rais Yoweri Museveni wa Uganda na Rais Hassan Sheikh Mohamud wa Somalia ambao nao wamethibitisha kushiriki katika mkutano huo.

Mkutano huo unafanyika wakati Umoja wa Mataifa ukisema takriban watu 900 wameuawa na wengine 2,880 kujeruhiwa katika mapigano ya hivi karibuni katika mji wa Goma, ambao umetekwa na waasi.

Mapigano hayo yameshuhudia mamia ya maelfu ya watu wakihama makazi yao katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, huku UN ikisema tangu kuanza kwa mwaka 2025, zaidi ya watu 400,000 wamehama makazi yao.

Wakati Jumuiya za Kimataifa zikimshutumu Rais wa Rwanda Paul Kagame kwa kushiriki katika machaafuko ndani ya DRC, mwenyewe amekataa hilo na kusema hajui kama wanajeshi wake wapo ndani ya nchi hiyo.

"Kuna mambo mengi sijui. Lakini ukitaka kuniuliza, kuna tatizo nchini Congo linaloihusu Rwanda? Na kwamba Rwanda ingefanya lolote kujilinda? Ningesema kwa asilimia 100," alisema Rais Kagame alipohojiwa na kituo cha CNN.

Ujio wa marais hao hapa nchini ni kuonyesha kwa kiwango gani Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyokubalika kimataifa katika masuala mbalimbali ikiwemo hili la DRC, ambalo limeshindwa kuwakutanisha Rais Kagame na Rais Tshisekedi kukaa meza moja.

# Siku ya wanawake kuwa ya kipekee

NA MWANDISHI WETU

**IMEELEZWA maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2025 yatakuwa kwa namna ya kipekee yakibeba sura ya kipekee kwa kuwa yanaambatana na miaka 30 ya utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing (1995).**

Hayo yamebainika jijini Dar Es Salaam wakati Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima alipokuwa akizungumzia Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2025.

Waziri Dkt. Gwajima amesema, kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ni Machi 8, 2025 ambapo kitaifa yatafanyika mkoani Arusha na kutatanguliwa na maadhimisho katika ngazi ya mikoa nchi nzima ili kuwa na ushiriki wa wanawake na jamii kwa wingi zaidi. Siku ya kilele, Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Katika mkutano huo wa Beijing yalifikiwa maazimio ambayo Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa imeendelea kutekeleza. Mwaka huu ni wa thelathini (30) tangu utekelezaji ulipoanza, hivyo mataifa yatatumia maadhimisho haya kutathimini utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing ikiwa pamoja na kuweka mikakati endelevu ya utekelezaji" amesema Waziri Dkt. Gwajima

Ameongeza kuwa wiki ya maadhimisho hayo Wizara, Taasisi za Umma na Binafsi na Makampuni zitatoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Vilevile kutakuwa na maonesho ya bidhaa za wajasiriamali mbalimbali hivyo ametoa rai kwa wananchi kujitokeza katika maeneo yao kupata huduma na kununua bidhaa mbalimbali.

Amesema kaulimbiu ya mwaka huu ni "Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji" ambayo imetokana na Kaulimbiu ya Kimataifa "For All Women and Girls. Equality. Rights. Empowerment". Lengo likiwa ni kuhamasisha jamii kukuza Usawa, Haki na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana na kwa kuzingatia kipindi hiki kuelekea uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ili, wajiamini, wajiandae na wajitokeze kugombea nafasi za uongozi.

Aidha Waziri Dkt. Gwajima amesema Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Sare maalum ya Kitaifa ambacho ni kitenge kwa ajili ya kuvaliwa siku ya kilele. Sare hiyo itasambazwa Mikoa yote na itapatikana kwa bei ya Sh. 25,000/= na haitazidi Sh. 30,000/= kwa rejareja kutegemeana na umbali wa mahali. Aidha, kabla ya kilele cha maadhimisho, mikoa itaadhimisha kwa Sare zao.

Amesisitiza Serikali kwa kutambua umuhimu wa siku hiyo inahimiza Wanawake na Wananchi kwa ujumla kujitokeza katika maadhimisho kwa kushiriki matukio yote kuanzia uzinduzi, maonesho na makongamano ili kuwa na maadhimisho yenye tija na mafanikio kwa ustawi na maendeleo ya Wanawake hapa nchini.

# Biashara Ya Urembo wa Kike Tanzania



NA MWANDISHI MAALUM

**BIASHARA ya kuuza bidhaa za urembo wa kike hapa nchini ni fursa yenye ukuaji mkubwa kutokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa za kujipamba, vipodozi, na vifaa vya urembo.**

Kuanzisha biashara hii kunahitaji mipango madhubuti, uelewa wa soko, na mikakati ya uendeshaji ili kuhakikisha mafanikio.

Hapa chini ni mwongozo wa hatua kwa hatua kuhusu jinsi ya kuanzisha na kuendesha biashara ya kuuza urembo wa kike kwa jumla na rejareja.

Hatua za Kuanzisha Biashara ya Kuuza Urembo wa Kike

**1. Utafiti wa Soko**

Utafiti wa soko ni hatua muhimu kabla ya kuanzisha biashara:

Mahitaji ya Wateja: Tambua mahitaji ya wateja wa bidhaa za urembo. Angalia aina za bidhaa wanazopendelea na viwango vya bei wanavyotaka.

Washindani: Chunguza washindani wako, wapi wanakauza, bei zao, na huduma wanazotoa. Elewa nguvu na mapungufu yao.

Trendi za Soko: Fuata mitindo ya urembo na bidhaa zinazojitokeza kama mpya kwenye soko.

**2. Mpango wa Biashara**

Mpango wa biashara utakuwa mwongozo wako katika kuanzisha na kuendesha biashara. Mpango huu unapaswa kujumuisha:

Muhtasari wa Biashara: Maelezo kuhusu biashara yako, malengo, na maono.

Utafiti wa Soko: Matokeo ya utafiti wako wa soko.

Mikakati ya Masoko: Jinsi utakavyovutia wateja na kuongeza mauzo.

Mpango wa Kifedha: Makadirio ya gharama, mapato, na jinsi utakavyopata mtaji wa kuanzisha biashara.

**3. Upatikanaji wa Mtaji**

Mtaji unahitajika kwa ajili ya kuanzisha biashara: Akiba Binafsi: Tumia akiba yako binafsi kuanzisha biashara. Mikopo: Tafuta mikopo kutoka benki au taasisi nyingine za kifedha. Uwekezaji: Tafuta wawekezaji wa kuwekeza katika biashara yako.

**4. Kupata Leseni na Vibali**

Leseni na vibali vya biashara ni muhimu: Leseni ya Biashara: Pata leseni kutoka Halmashauri ya Jiji/Mji ili kuwa na ruhusa ya kufanya biashara.

Vibali vya Afya: Ikiwa unahitaji kuhifadhi au kuuza bidhaa zinazohitaji viwango vya afya, hakikisha unapata vibali vya afya.

Vibali vya Usalama: Tafuta vibali vya usalama kama inavyohitajika kwa ajili ya matumizi ya vifaa vya biashara yako.

**5. Kuandaa Eneo la Biashara**

Chagua eneo bora kwa biashara yako: Eneo la Mauzo: Tafuta maeneo yenye watu wengi kama vile masoko, vituo vya biashara, na maeneo yenye mtindo wa maisha wa juu.

Vifaa vya Mauzo: Nunua vifaa kama vile shelfu za kuonesha bidhaa, meza, na vifaa vya kuhifadhi bidhaa.

Kuanza Biashara ya Kuuza Urembo wa Kike

**Kupata Vifaa na Malighafi**

Nunua vifaa na malighafi muhimu: Bidhaa za Urembo: Pata bidhaa za urembo za ubora mzuri kutoka kwa wauzaji wa malighafi. Hakikisha kuwa bidhaa hizo zina ithibati ya afya na usalama.

Vifaa vya Mauzo: Nunua vifaa kama vile vitambaa vya kupamba, shelfu za kuonesha bidhaa, na vifaa vya usafi.

Vifaa vya Usafi: Hakikisha unapata vifaa vya usafi kama vile mikono ya usafi, sabuni, na vifaa vya kuosha.

**Kuajiri Wafanyakazi**

Ajiri wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu:

Wafanyakazi wa Mauzo: Ajiri watu wenye ujuzi wa mauzo na huduma kwa wateja. Wafanyakazi hawa wanapaswa kuwa na uelewa wa bidhaa za urembo.

Wafanyakazi wa Usafi: Ajiri wafanyakazi wa usafi ili kuhakikisha mazingira ya biashara yako ni safi na salama.

**Matangazo na Masoko**

Tumia mikakati bora ya masoko ili kuvutia wateja: Matangazo: Tumia vipeperushi, mabango, na mitandao ya kijamii kutangaza biashara yako. Tafuta njia za kuufikia umma.

Huduma Bora kwa Wateja: Hakikisha unatoa huduma bora kwa wateja na kuwajali ili wawe wateja wa kurudi.

Mikakati ya Mauzo: Tumia mikakati kama ofa, punguzo, au zawadi za mara kwa mara ili kuvutia wateja.

**Kudhibiti Gharama na Mapato**

Kudhibiti gharama na mapato ni muhimu: Uhasibu: Rekodi mapato na matumizi kwa uangalifu ili kujua faida na hasara.

Usimamizi wa Malighafi: Hakikisha malighafi zako zinahifadhiwa kwa usalama na zinatumika kwa ufanisi.

Mikakati ya Kuuza Urembo wa Kike

**Uendelezaji na Matangazo**

Matangazo ni muhimu kwa kuongeza mauzo:

Matangazo ya Kulipia: Tumia matangazo ya kulipia kwenye mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram, na Google Ads.

SEO: Hakikisha tovuti yako (ikiwa ipo) ina maneno muhimu (keywords) ili iweze kupatikana kwa urahisi kwenye injini za utafutaji kama Google.

Mikakati ya Mitandao ya Kijamii: Jenga uwepo mzuri kwenye mitandao ya kijamii kwa kutumia picha nzuri, video, na hadithi zinazovutia.

**Huduma kwa Wateja**

Huduma bora kwa wateja ni muhimu: Majibu ya Haraka: Jibu maswali na maombi ya wateja haraka kupitia barua pepe, chat, au simu.

Kurudisha na Kubadilisha: Toa sera rahisi na yenye ufanisi kwa kurudisha na kubadilisha bidhaa.

Maoni na Tathmini: Hifadhi sehemu ya maoni na tathmini kwenye tovuti yako au mitandao ya kijamii ili wateja waweze kutoa maoni na ushauri.



## MAONI

# Rais Samia anastahili pongezi

**HIVI karibuni Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema kuwa Mpango Mahsusi wa Kitaifa kuhusu Nishati (National Energy Compact) uliozinduliwa unalenga kuiwezeseha Tanzania kuunganisha umeme kwa kaya milioni 8.3 zaidi ifikapo mwaka 2030.**

Rais Dkt. Samia aliyasema hayo wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika kuhusu Nishati uliofanyika kwa muda wa siku mbili katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere, Dar es Salaam na kumalizika juzi.

Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano huo uliohudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka Burundi, Botswana, Congo, Comoros, Djibouti, Ethiopia, Gabon, Ghana, Guinea Bissau, Kenya, Lesotho, Liberia, Libya, Madagascar, Malawi, Mauritania, Nigeria, Sierra Leone, Somalia na Zambia.

Vile vile, mkutano huo ulihudhuriwa na Wawakilishi wa Wakuu wa Nchi na Serikali, Wakuu wa Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, Mashirika ya Kimataifa, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa lengo la kuongeza kasi ya usambazaji umeme barani Afrika ili kuwaunganisha watu milioni 300 na umeme katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Rais Dkt. Samia alisema kuwa kwa kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa nishati ya umeme, mkutano huo ulioandaliwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika utawezesha kuleta mageuzi ya kiuchumi, kukua kwa viwanda, kupunguza umaskini na kuimarisha ustawi wa watu.


Mkutano huo ulifanikiwa kupata ahadi za ufadhili wa Dola za Marekani Bilioni 40 kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa umeme barani Afrika. Aidha, jumla ya nchi za Afrika 12 zimeingia kwenye Mipango Mahsusi wa Kitaifa kuhusu Nishati.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa kupitia Mpango Mahsusi kuhusu Nishati, Tanzania inakusudia kuvutia mitaji na uwekezaji zaidi itakayowezesha kuongeza uzalishaji wa umeme nchini na kukukamilisha kuunganisha Mtandao wa Umeme wa Tanzania na nchi jirani ili kuwezesha biashara ya kuuza na kununua nishati hiyo.

Mpango huo utawezesha Serikali kukamilisha usambazaji umeme katika Vitongoji vyote 64,359 nchini ifikapo 2030. Vilevile, Mpango huo utapandisha kiwango cha uunganishaji wa umeme kutoka 46% ya sasa hadi kufikia 75%.

Kwetu Rais Dkt. Samia ambaye amekuwa kinara wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, alifurahisha wengi kwa kuweka bayana kuwa mpango huo wa nishati pia utasaidia kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, ikiwemo gesi asilia na majiko banifu.

Kila la kheri Rais Dkt. Samia katika mpango mkakati huo na tunaamini kwa dhati kabisa utafanikiwa katika hili, sisi tutaendelea kukuunga mkono ili utimize hili kwa Watanzania.




## FIKRA YA MJASIRIAMALI

# Zingatia hili unaposaka mtaji wako

**JINSI ya kupata mtaji wa biashara Tanzania ni muhimu sana kwa kuwa watu wengi huanzisha biashara kwa lengo la kupata pesa ila huwa ni ngumu sana kupata mtaji.**

Mara kadhaa nimekuwa nikieleza kuwa kuweka akiba kuna manufaa mengi, ikiwemo kupata uwezo wa kuwahi fursa mbalimbali na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Hivyo basi, unaweza kutunza kiasi fulani cha pesa katika kipato chako hatakama ni kidogo, ili uweze kupata mtaji wa kuanzisha biashara au mradi wako.

Nimewahi kukutana na watu kadhaa wakilalamika kuwa hawana mtaji, lakini ukiwachunguza sana utagundua kuwa wamezungukwa na mitaji mikubwa wasiyoitambua.

Hakuna haja yoyote ya kuwa na simu, televisheni, Kompyuta, na nguo za thamani kubwa wakati hauna mtaji wa kutekeleza mradi wako.

Unaweza kuuza vitu vyote ambavyo ukivikosa hutokufa ili uweze kupata mtaji; kumbuka uwekezaji ni muhimu kuliko maisha ya kifahari na anasa.

Ikumbukwe kuwa ukiwekeza utaweza kutengeneza pesa nyingi zaidi na kumudu kununua vitu vingine bora zaidi huko mbeleni.

Ikiwa una mahusiano mazuri na ndugu zako, wanafamilia au marafiki, kwanini unaona shida kuwaomba wakuwezeshe kupata mtaji?

Andaa wazo vizuri, tafuta watu au marafiki wakaribu watakaokuamini, waombe wakuwezeshe kupata mtaji na uwaahidi utaurejesha mapema kadri uwezavyo ili wakuamini

Faida za mtaji au mkopo kutoka kwa marafiki na ndugu: Mara nyingi hakuna riba. Hakuna masharti na vigezo vigumu.

Upatapo shida katika biashara au mradi wako ni rahisi ndugu kukuelewa. Kumbuka! Usicheze na mtaji wa biashara au mradi kwa kuwa umeupata kutoka kwa ndugu au marafiki; pia kumbuka kuwa mwaminifu kutimiza mapatano ili wakati mwingine usaidike.

Hivi leo kuna taasisi na mashirika mbalimbali yanayotoa mitaji ya fedha na vifaa kwa wajasiriamali mbalimbali ili waweze kutekeleza mawazo yao.

Hivi leo kuna taasisi na mashirika mbalimbali yanayotoa mitaji ya fedha na vifaa kwa wajasiriamali mbalimbali ili waweze kutekeleza mawazo yao.

Fuatilia vyombo mbalimbali vya habari pia jiunge na vikundi vya wajasiriamali wengine ili zitokeapo fursa za mitaji uweze kuzifahamu na kuzitumia.

Hivi leo ziko taasisi kedekede zinazotoa mikopo kwa ajili ya watu mbalimbali; hivyo, mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha inaweza kutumiwa kama mtaji mzuri sana wa biashara.

Hata hivyo nimekuwa nikiwashauri wajasiriamali wengi hasa wachanga kutokupendelea njia hii, ikiwa hawajaweka mikakati sahihi ya kutumia na kurejesha mkopo husika.

Hakikisha kama unataka kutumia njia hii kupata mtaji wa biashara au mradi wako, umejipanga vyema na unafahamu wazi njia na mbinu utakazozitumia kurejesha mkopo wa taasisi husika hata kama mambo yatakwenda mrama.

**Tukutane kesho**

# Kanuni za Kufanikiwa Kimaisha

NA MWANDISHI WETU

**KUFANIKIWA kimaisha kunajumuisha mambo mengi zaidi ya utajiri wa kifedha pekee. Mafanikio yanahusu ustawi wa jumla, kutimiza malengo yako ya binafsi, kitaaluma, na kijamii, huku ukifurahia furaha ya kweli na utulivu.**



Hapa kuna baadhi ya kanuni ambazo zinaweza kukusaidia kufikia mafanikio katika maisha yako kwa ujumla.

**1. Weka Malengo Yenye Maana**

Kuwa na malengo ni msingi wa mafanikio katika maisha. Bila kuwa na mwelekeo au dira ya nini unataka kufanikisha, ni rahisi kupoteza mwelekeo na kushindwa kufanya maendeleo.

Weka malengo ya muda mfupi na muda mrefu: Malengo ya muda mfupi yatakusaidia kushinda changamoto za kila siku, huku ya muda mrefu yakikuongoza kufikia ndoto zako.

Andika malengo yako: Andika malengo yako ili yawe wazi na yaweze kufuatiliwa. Kuweka malengo kwenye maandishi kunakuongezea uwajibikaji.

**2. Fanya Kazi kwa Nidhamu na Bidii**

Nidhamu binafsi ni jambo la msingi kwenye safari ya mafanikio. Watu waliofanikiwa hufanya kazi kwa bidii na kufuata mipango yao bila kuacha kazi kwenye matumaini ya bahati.

Zingatia kazi yako kwa ubora: Kila kitu unachofanya, kifanye kwa ubora. Ubora huleta mafanikio, na kutofanya hivyo kunaweza kukuzuia kufika kileleni.

Jifunze kujituma hata kama hali sio nzuri: Ni rahisi kufanya kazi ukiwa na motisha, lakini watu waliofanikiwa hujua kufanya kazi hata wanapokosa nguvu ya kufanya hivyo.

**3. Jifunze Kila Siku**

Elimu ni ufunguo wa mafanikio. Kujifunza si lazima kuwe ni rasmi tu kama darasani, bali hata kutoka kwa vitabu, mafunzo mtandaoni, au kutoka kwa watu waliofanikiwa.

Panua maarifa yako kila siku: Soma vitabu, makala, au jifunze stadi mpya zinazoweza kusaidia kuboresha maisha yako.

Jifunze kutokana na makosa: Mafanikio mara nyingi yanatokana na kujifunza kutokana na kushindwa. Usikate tamaa unapokosea; badala yake, tafuta funzo lililojificha nyuma ya makosa hayo.

**4. Kuwa na Mtazamo Chanya**

Mtazamo chanya unakuza uwezekano wa kufanikiwa. Hata unapokutana na changamoto kubwa, kuwa na mtazamo chanya hukuwezesha kuona fursa badala ya vikwazo.

Fikiria kwa matumaini: Badala ya kuangalia mambo hasi au matatizo, jifunze kuona njia za kutatua matatizo.

Jizoeze shukrani: Shukuru kwa kila mafanikio madogo unayopata, kwani hii inakupa motisha ya kuendelea mbele.

**5. Kuwa na Mipango Thabiti**

Mipango ni nguzo muhimu katika mafanikio ya muda mrefu. Bila mipango thabiti, ni rahisi kuvurugika na kupoteza lengo lako kuu.

Panga kila siku au wiki yako: Kuwa na ratiba inayoeleweka ya majukumu yako inakusaidia kufuatilia maendeleo na kuhakikisha unakamilisha kazi zako.

Rekebisha mipango yako inapobidi: Mipango inaweza kubadilika kutokana na mazingira, hivyo uwe tayari kurekebisha mikakati yako inapohitajika.

**6. Simamia Fedha kwa Hekima**

Fedha ni sehemu muhimu ya mafanikio, na jinsi unavyosimamia fedha zako inaathiri sana ubora wa maisha yako kwa ujumla.

Jifunze kuweka akiba na kuwekeza: Uwekezaji na kuweka akiba ni msingi wa kujenga utajiri wa muda mrefu. Hata kipato kidogo kinaweza kukua ikiwa kitasimamiwa kwa busara.

Epuka madeni yasiyo ya lazima: Mikopo inaweza kuwa mizigo ikiwa hutatumia kwa busara. Epuka mikopo isiyo na manufaa makubwa kwa mustakabali wako wa kifedha.

**7. Fanya Kazi na Watu Wenye Maono Kama Wewe**

Marafiki, familia, na washirika wako wanaweza kuwa na athari kubwa katika safari yako ya kufanikiwa. Kujizunguka na watu wenye mitazamo chanya na wanaolenga mafanikio husaidia kuimarisha maono yako.

Tafuta watu wenye maono sawa na yako: Kushirikiana na watu wenye lengo la mafanikio husaidia kujenga mtandao mzuri na kuongeza motisha ya kusonga mbele.

Tengeneza mtandao wa watu wenye mafanikio: Marafiki na washirika wenye maono na ujuzi wanakusaidia kuona fursa zaidi na hata kutoa msaada muhimu wa kiakili au kifedha.

**8. Kuwa na Uvumilivu na Ustahimilivu**

Mafanikio ya kweli hayaji mara moja, yanahitaji uvumilivu. Mchakato wa kujenga mafanikio ni mrefu, na changamoto nyingi hujitokeza njiani.

Kumbuka kuwa mafanikio ni safari: Kila hatua ni muhimu. Usikate tamaa pale mambo yanapokuwa magumu; badala yake, tambua kwamba kila kikwazo ni sehemu ya safari yako ya mafanikio.



# Unapohaha Kupata Mkopo wa Biashara

NA MWANDISHI WETU

**Kupata mkopo wa biashara ni njia muhimu ya kupata mtaji wa kuanzisha au kukuza biashara yako.**

Hata hivyo, kupata mkopo si jambo la moja kwa moja; unahitaji kufuata hatua muhimu, kuwa na mpango thabiti, na kujiandaa ili uweze kufanikiwa katika maombi yako.

Hapa chini ni mwongozo wa jinsi ya kupata mkopo wa biashara.

**1. Tambua Aina ya Mkopo Unayohitaji**

Kabla ya kuanza mchakato wa kuomba mkopo, ni muhimu kujua ni aina gani ya mkopo unahitaji na kwa nini. Unaweza kuwa unahitaji mkopo wa muda mfupi au mrefu, na kila mkopo una masharti tofauti.

**Mkopo wa Muda Mfupi**

Huu ni mkopo unaotolewa kwa muda mfupi, kwa kawaida miezi hadi mwaka mmoja.

Unafaa kwa gharama za dharura au kununua mali za biashara zinazohitajika haraka, kama vile bidhaa au vifaa vya ofisini.

**Mkopo wa Muda Mrefu**

Mkopo wa muda mrefu unaweza kutolewa kwa miaka kadhaa na ni mzuri kwa miradi mikubwa kama vile kununua mali isiyohamishika au mitambo ya uzalishaji.

Mkopo Bila Dhamana

Ni mkopo ambao hauhitaji kuweka dhamana kama mali au nyumba. Kwa kawaida, riba yake ni ya juu zaidi kwani mkopeshaji anachukua hatari kubwa zaidi.

**Mkopo wa Dhamana**

Mkopo wa dhamana unahitaji kuweka mali kama dhamana ya mkopo. Kwa sababu ya dhamana hiyo, mkopo huu kwa kawaida una riba ya chini.

2. Andaa Mpango wa Biashara

Mpango wa biashara ni nyenzo muhimu ya kuonesha mkopeshaji kuwa una mpango madhubuti wa kuendesha biashara yako.

Mpango huu unaonyesha jinsi utakavyotumia mkopo huo na jinsi utakavyorejesha pesa.

**Maelezo ya Biashara Yako**

Eleza ni aina gani ya biashara unaendesha au unataka kuanzisha. Eleza kwa nini unahitaji mkopo, kiasi gani unahitaji, na jinsi utakavyotumia fedha hizo.

**Uchambuzi wa Soko**

Onyesha kuwa umefanya utafiti wa soko lako na kuelewa wateja wako na washindani.

Hii itasaidia kuwapa mkopeshaji uhakika kuwa biashara yako ina uwezo wa kukua.

**Makadirio ya Mapato**

Weka makadirio ya mapato na faida unayotarajia kupata. Pia, onyesha ni jinsi gani utaweza kurejesha mkopo kwa wakati.

**3. Andaa Nyaraka Muhimu**

Kuna nyaraka kadhaa ambazo taasisi za kifedha zitahitaji kabla ya kukupatia mkopo wa biashara.

Hizi nyaraka ni muhimu kuhakikisha kuwa una sifa za kuaminika kifedha.

Rekodi ya Kifedha ya Biashara

Ikiwa tayari unaendesha biashara, utahitaji kuwasilisha rekodi za kifedha kama vile mapato ya kila mwezi au kila mwaka.

Hii itawapa mkopeshaji wazo la jinsi biashara yako inavyoendeshwa.

**Taarifa za Akaunti ya Benki**

Benki au taasisi za mikopo zinaweza kuhitaji kuona taarifa za akaunti ya benki yako kwa kipindi fulani, kwa kawaida miezi 6 hadi mwaka mmoja, ili kuangalia hali ya kifedha ya biashara yako.

Taarifa za Deni au Mikopo Mengine

Ikiwa tayari una mikopo mingine, taasisi za kifedha zitahitaji kujua taarifa hizo.

Hii ni pamoja na kiasi cha mkopo kilichobaki na kiwango cha riba unacholipa.

**Dhamana**

Kama unatafuta mkopo wa dhamana, utahitaji kuonesha mali utakayoweka kama dhamana, kama vile nyumba, gari, au mali nyingine.

**4. Angalia Sifa Zako za Mkopo**

Taasisi za kifedha zitachunguza historia yako ya mkopo ili kujua kama una sifa nzuri za kukopesheka. Hii inahusisha taarifa kuhusu mikopo uliyowahi kuchukua na jinsi ulivyolipa.

**Kagua Ripoti Yako ya Mikopo**

Ni vyema kuangalia ripoti yako ya mikopo kabla ya kuomba mkopo. Unaweza kufanya hivyo kupitia ofisi za mikopo ili kuhakikisha hakuna makosa au taarifa mbaya.

**Kurekebisha Dosari**

Ikiwa una deni kubwa au historia mbaya ya mikopo, fanya juhudi za kurekebisha hali hiyo kabla ya kuomba mkopo.

Hii inaweza kujumuisha kulipa madeni ya zamani au kuimarisha mtiririko wa mapato yako.

**5. Tafuta Benki au Taasisi Sahihi**

Kuna taasisi nyingi zinazotoa



mikopo ya biashara, ikiwemo benki, vyama vya ushirika, na taasisi ndogo za kifedha. Kila moja ina masharti tofauti, hivyo ni muhimu kutafuta inayokidhi mahitaji yako.

**Benki za Kibiashara**

Benki kubwa zinaweza kuwa na urasimu zaidi, lakini zinatoa mikopo mikubwa kwa biashara zenye uwezo wa kifedha.

Vyama vya Ushirika au Taasisi za Kifedha Ndogo

Taasisi hizi mara nyingi zinatoa mikopo kwa biashara ndogo ndogo na zina masharti laini kuliko benki kubwa.

Vyama vya ushirika vinaweza pia kutoa mikopo bila dhamana kwa wanachama wake.

**Watoa Mikopo ya Kielektroniki**

Katika ulimwengu wa sasa, kuna watoa mikopo wa mtandaoni wanaotoa mikopo haraka na kwa urahisi.

Hawa mara nyingi hawana masharti mengi kama benki za kawaida, lakini wanaweza kuwa na viwango vya riba vya juu.

**6. Angalia Masharti ya Mkopo**

Kila mkopo unakuja na masharti yake. Unahitaji kuelewa masharti hayo vizuri kabla ya kukubali mkopo.

Kiwango cha Riba

Kiwango cha riba ni gharama unayolipa kwa ajili ya mkopo. Hakikisha unaelewa ni kiasi gani cha riba utakacholipa kwa muda wa mkopo.

**Muda wa Kulipa Mkopo**

Fahamu ni muda gani utakaotumia kulipa mkopo. Mikopo ya muda mrefu inakuja na malipo madogo kila mwezi, lakini inaweza kuwa na riba kubwa kwa jumla.

# Trump 'aitafakarisha' Dunia kwa kuifunga USAID



**MTEGEMEA CHA NDUGU? Mithali hii inataka kuzitokea nchi nyingi duniani haswa baada ya mustakabali wa Serikali ya Marekani kutoa misaada kwa mataifa ya nje sasa upo shakani, huku wafanyikazi wa mashirika ya misaada wakitakiwa wasiingie kazini huku utawala wa Donald Trump ukifanya yake.**

Trump anataka kulifunga Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa (USAID), huku akitaka lifanye kazi kama Idara ya Serikali, lakini mpango huu unahusisha kupunguzwa kwa kiasi kikubwa cha fedha na wafanyakazi wake, ndani ya shirika hilo.

Jumatatu wiki hii, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Marco Rubio, alikosoa uongozi wa USAID kwa 'kutokuwa na nidhamu' na kusema kwamba yeye ndiye 'kiongozi wa muda' wa shirika hilo.

Rais wa Marekani, Donald Trump, na mmoja wa washauri wake wakuu, bilionea Elon Musk, wamekuwa wakikosoa vikali shirika hilo. Hatua ya kufunga shirika hili inaweza kuwa na athari kubwa kwa programu za kibinadamu duniani kote.

Ni nini USAID na majukumu yake ni yapi?

USAID lilianzishwa miaka ya 1960 ili kusimamia programu za misaada ya kibinadamu kwa niaba ya Serikali ya Marekani duniani kote. Limeajiri takriban watu 10,000 wawili kati ya watatu wakifanya kazi nje ya nchi.

Hata hivyo, kazi nyingi za kiutendaji hufanywa na mashirika mengine ambayo yamepewa mikataba na kupatiwa fedha na USAID. Shughuli zake ni nyingi.

Kwa mfano, sio tu kwamba USAID hutoa chakula katika nchi ambapo watu wanateseka na njaa, pia linaendesha mfumo wa upimaji wa kiwango cha njaa duniani, unaotumia uchambuzi wa data kujaribu kutabiri maeneo ambayo upungufu wa chakula unaibuka.

Bajeti kubwa ya USAID hutumika kwa programu za afya, kama vile kutoa chanjo za polio katika nchi ambazo hukumbwa na ugonjwa huo hatari na kusaidia kukabiliana na virusi hivyo ambavyo huenda vikaleta majanga ulimwenguni.

Isitoshe mfuko wa msaada wa kimataifa wa BBC Media Action, ambao hufadhiliwa na mashirika mbalimbali, hupokea ufadhili kutoka USAID.

Kulingana na data za Serikali, Marekani iligharamika dola bilioni 68 katika misaada ya kimataifa mwaka 2023.

Jumla ya fedha hizo zimegawanyishwa kwa mashirika na idara mbalimbali, lakini bajeti ya USAID inajumlisha zaidi ya nusu ya fedha hizo ikipokea takriban dola bilioni 40.

Fedha nyingi hutumika katika bara Asia, mataifa ya Afrika yaliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara na Ulaya hasa katika juhudi za kibinadamu nchini Ukraine. Marekani ni taifa ambalo linaongoza kufadhili misaada ya kimataifa duniani. Uingereza ikiwa nafasi ya nne kufadhili misaada ya kimataifa hasa katika shughuli za kibinadamu.

Kwanini Trump, Elon Musk hawalitaki?

Trump ni mkosoaji wa muda mrefu wa Marekani kutumia fedha zake kufadhili mataifa mengine akisema hauwakilishi thamani kwa kodi wanazotoa Wamarekani.

Amekosoa vikali USAID, akielezea viongozi wake wa juu kama 'watu wasiojielewa'. Kufunga shirika hili kutaweza kupigiwa upatu kutoka kwa wamarekani.

Tafiti za maoni kwa muda mrefu zimeonyesha kuwa wapiga kura wa Marekani wanapendelea serikali yao kupunguza matumizi ya misaada ya kigeni.

Kwa mfano, moja ya hatua za kwanza alizochukua Trump alipochaguliwa tena ilikuwa kusaini agizo la kiutendaji linalohusisha kusitisha takriban matumizi yote ya kimataifa kwa muda wa siku 90 ili kupitia upya matumizi hayo.

Notisi ikatolewa ikisitisha shughuli zinazoendelea zisimamishwe mara moja.

Muda mchache baadaye agizo likatolewa kuwa baadhi ya programu za kibinadamu ziendelee, ingawa agizo la awali lilikuwa limevuruga shughuli kadhaa kote ulimwenguni.

Elon Musk na Donald Trump wamekuwa wakikosoa vikali matumizi ya Marekani nje ya nchi, pamoja na programu ambazo hutoa misaada ya dawa katika nchi maskini na pia kufadhili miradi ya maji zilisitishwa kwa haraka.

Mkwaruzano kati ya Ikulu ya Marekani na USAID ulichemka zaidi baada ya wafanyakazi wa USAID kukatazwa kuingia afisini au kufikia data za kifedha katika makao makuu yake.

Mapema wiki hii Elon Musk kupitia mtandao wa X alisema kuwa suala la kusitisha programu za USAID alishauriana na rais kwa kina na kuamua inapaswa kufungwa.

Marco Rubio amethibitisha kuwa programu nyingi za USAID zitaendelea lakini zitalingana na maslahi ya taifa.

Ingawa ni wazi kwamba Ikulu ya White House ina ushawishi mkubwa kwa USAID, nguvu hiyo kisheria ni ndogo. USAID iliundwa baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Misaada ya Kigeni mwaka 1961.

Sheria hiyo ilimtaka Rais wa Marekani kuanzisha shirika ambalo lingesimamia matumizi ya fedha nje ya nchi. Rais John F. Kennedy alianzisha USAID kwa amri ya kiutendaji.

Trump hawezi kusitisha shughuli za USAID kwa kutia saini agizo la kiutendaji na akichukua mkondo huo zaidi atakabiliwa na mashtaka chungu nzima katika mahakama na bungeni.

Miongoni mwa shughuli za dharura zilizokuwa zikitekelezwa na USAID ni kutuma vifaa vya utafutaji na uokoaji nchini Uturuki baada ya tetemeko kuu la ardhi

Kufunga kabisa USAID kutahitaji hatua ya Bunge, ambapo Chama cha Republican cha Trump kinashikilia wingi wa wabunge katika mabunge yote mawili.

Athari za kufunga USAID

Kwa kuwa Marekani inatoa kiasi kikubwa cha misaada ya kimataifa, mabadiliko yoyote katika jinsi fedha hizo zinavyotumika yataonekana kote duniani.

USAID inahusika katika shughuli mbalimbali, kutoka kutoa viungo bandia kwa majeruhi wa kivita nchini Ukraine, hadi kutoa msaada wa kupambana na virusi vya Ebola Afrika.

Baada ya kusitishwa kwa matumizi ya kimataifa kwa siku 90, Marco Rubio alisema kuwa 'kila dola' lazima 'ithibitishwe' kwa ushahidi kuwa inafanya Marekani kuwa salama, yenye nguvu na yenye ustawi zaidi."

Pia kuna maswali kuhusu ni kiasi gani Marekani itatumia ng'ambo katika miaka ijayo, kama Musk akiwezeshwa na Trump anajaribu kupunguza mabilioni kutoka kwa bajeti ya serikali.

# Jinsi Ya Kuwa Mjasiriamali Mwenye Mafanikio

NA MWANDISHI MAALUM

**UJASIRIAMALI ni safari ya kusisimua inayoweza kukuwezesha kujitegemea kifedha na kutoa mchango mkubwa kwa jamii. Hata hivyo, kuwa mjasiriamali mwenye mafanikio kunahitaji ujuzi, nidhamu, na mbinu za kipekee.**

Kama unavyoweza kuhitaji motisha na mwongozo wa kivitendo, hapa kuna hatua muhimu na mbinu za kuwa mjasiriamali aliyefanikiwa.

**1. Tambua Wazo la Biashara**

Wazo la biashara ni msingi wa safari yako ya ujasiriamali. Ili kuwa mjasiriamali mwenye mafanikio, unahitaji kuwa na wazo bora la biashara ambalo linaendana na soko unalolenga.

**Chagua Biashara Yenye Fursa**

Fanya utafiti wa kina ili kuelewa ni biashara gani inayo mahitaji makubwa kwenye soko, lakini pia ambayo unaipenda. Biashara yenye fursa ni ile ambayo watu wanahitaji huduma au bidhaa zake mara kwa mara.

**Tambua Suluhisho la Tatizo**

Wajasiriamali wengi waliofanikiwa walitambua tatizo fulani katika jamii na kulipatia suluhisho. Uliza maswali kama: "Ni changamoto gani watu wanakabiliana nazo?" na "Ninaweza kuwasaidiaje?"

**Wekeza Katika Wazo**

Usijaribu kuanzisha biashara kwa sababu tu inaonekana kuwa maarufu au faida. Hakikisha unaelewa vizuri sekta unayotaka kuingia ili uwe na nafasi bora ya kufanikiwa.

2. Andaa Mpango Biashara

Mpango wa biashara ni ramani yako ya mafanikio. Inakupa mwelekeo sahihi wa jinsi utakavyofanikisha wazo lako na kupata faida.

Mpango huu unaonyesha mikakati ya kifedha, masoko, na mipango ya muda mfupi na mrefu.

**Eleza Lengo la Biashara**

Ni muhimu kuelewa ni malengo gani unataka kufanikisha kupitia biashara yako. Je, unalenga soko la ndani au kimataifa? Lengo hili litaongoza hatua zako za baadaye.

**Tathmini Mahitaji ya Mtaji**

Kila biashara inahitaji mtaji wa kuanzia. Fanya hesabu za awali za gharama za kuanzisha na kuendesha biashara yako kwa miezi kadhaa bila faida. Hii itakusaidia kufahamu kiasi cha pesa unachohitaji.

**Tengeneza Mkakati wa Masoko**

Ukiwa na bidhaa nzuri, unahitaji pia kujua jinsi ya kuiuza. Tengeneza mpango wa masoko unaojumuisha mbinu za kuwafikia wateja wako, kama vile matangazo ya mtandaoni, mitandao ya kijamii, au mabango.

**3. Jifunze Ujuzi wa Kijasiriamali**

Ujasiriamali ni mchakato unaohitaji ujuzi wa aina nyingi. Unahitaji kuelewa mambo ya usimamizi wa fedha, uuzaji, mawasiliano, na uongozi.

Kusoma na Kujifunza Mara kwa Mara

Kuwa mjasiriamali mwenye mafanikio kunahitaji kuwa mwanafunzi wa maisha. Kusoma vitabu na kujifunza kutoka kwa wengine kutakupa maarifa na ujuzi muhimu.

**Jifunze Usimamizi wa Fedha**

Fedha ni sehemu kubwa ya mafanikio ya biashara. Jifunze jinsi ya kusimamia bajeti yako, kudhibiti mapato na matumizi, na kuwekeza faida kwa busara. Wateja ndio kiini cha biashara yoyote.

Jifunze jinsi ya kuwavutia wateja, kuhifadhi wateja wa zamani, na jinsi ya kujenga uhusiano wa kudumu nao.

**4. Jenga Mitandao ya Mahusiano**

Kujenga mitandao ya watu ni muhimu kwa ujasiriamali. Mahusiano mazuri yanaweza kusaidia kupata fursa, wateja, na hata wawekezaji.

**Hudhuria Mikutano ya Biashara**

Kushiriki katika mikutano, warsha, na hafla za biashara kunakupa nafasi ya kukutana na watu wengine wenye maono kama yako.

Watu hawa wanaweza kukusaidia kwa ushauri, ushirikiano, au hata kuwa wateja wako wa kwanza.

Shirikiana na Watu Wenye Mafanikio

Kutafuta ushirikiano na wajasiriamali wenye uzoefu ni njia bora ya kujifunza mbinu bora za mafanikio. Wanaweza pia kukuunganisha na watoa huduma au wateja muhimu.

**5. Kuwa na Nidhamu na Bidii ya Kazi**

Mafanikio ya biashara yoyote yanahitaji nidhamu kali na bidii. Bila juhudi kubwa na kujitoa, ni vigumu kufikia malengo yako ya kibiashara.

**Weka Ratiba ya Kazi**

Wajasiriamali waliofanikiwa wanajua jinsi ya kudhibiti muda wao vizuri. Unda ratiba ya kila siku inayokuwezesha kufanikisha majukumu yako muhimu. Hakikisha unatumia muda wako kwa kazi za kipaumbele.





# Unapotaka kufuga samaki wa kambale

NA MWANDISHI MAALUM

**UFUGAJI wa kambale kwa hapa nchini ni mzuri, pia samaki wa kambale hupendwa na watu wengi kwa kuwa nyama yake ina ladha nzuri na ni laini.**

Kambale huzaliana vizuri zaidi wanapokuwa mtoni au sehemu ambayo wanapata tope.

Pia mfugaji anapokusudia kufuga aina hii ya samaki kibiashara, ni lazima kusakafia bwawa ili kuepuka uharibifu unaoweza kusababishwa na samaki hawa.

**Umbile la Samaki wa Kambale**

Samaki aina ya kambale wana umbo refu, mpana kuanzia shingoni, ingawa kichwa ni kidogo, na upande wa mkia ni mwembamba. Samaki hawa wana rangi ya kijivu na wengine nyeusi.

**Kulisha Samaki wa Kambale**

Unaweza kulisha kambale kwa kutumia unga wa samaki, maharagwe yaliyosagwa, mahindi, mchele pumba, ngano na bidhaa nyingine.

Unaweza kujenga mfumo ambao utawawezesha samaki hawa kupata aina mbalimbali za wadudu, pamoja na majani, ili kusaidia wapate mlo kamili.

**Ukuaji na Uvunaji wa Kambale**

Aina hii ya samaki, wakitunzwa vizuri, wanaweza kukua kwa haraka na kuwa na uzito mzuri unaoweza kumpatia mfugaji faida nzuri.

Unaweza kuanza kuvuna kambale baada ya miezi sita tangu walipopandikizwa kwenye bwawa.

**Jinsi Ya Kutafuta Soko La Kambale**

Wafugaji walio wengi, wamekuwa wakianzisha miradi ya ufugaji wa samaki kwa kufuata mkumbo bila kutambua kwanza soko watakalozalishia samaki hao.

Jambo hili huwafanya wafugaji kuwa na kipato kidogo tofauti na nguvu waliyotumia kuzalisha.

Inapofikia wakati wa kuvuna samaki, kiasi kikubwa huuzwa papo hapo bila kufika kwenye soko halisi, jambo linalosababisha kipato kuwa duni.

Ni vyema mfugaji akawa na soko maalumu ambalo atazalishia. Unaweza kuzalisha kwa ajili ya shule, hospitali, vyuo, au taasisi yoyote.

Ni vizuri kuzingatia yafuatayo kabla ya kuanza uzalishaji wa samaki. Fahamu ni aina gani ya samaki inayopendwa zaidi katika eneo ulipo. Samaki wanaopendwa wanatakiwa wawe na ukubwa gani. Kiasi cha samaki kinachohitajika katika soko ulipo. Ni kipindi gani ni kizuri kwa uvunaji wa samaki. Ni wakati gani mzuri wa kuuza samaki.

Je, katika eneo lako kuna mfugaji mwingine anaezalisha samaki kwa ajili ya soko hilo? Bei ya aina ya samaki unaozalisha ikoje?

**Jinsi Ya Kuwasikiliza Wateja wa Kambale**

Wakati wote mfugaji anapouza samaki, ni lazima kusikiliza kwa umakini, wateja wako wanasemaje.

Je, wanapendelea samaki unaouza. Je, samaki wako ni wadogo sana au ni wakubwa sana. Wakija kununua wananunua kwa kiasi gani, kikubwa au kidogo. Je, wanapendelea uzalishe zaidi? Je, kuna wafanyabiashara wanataka uzalishe zaidi ili nao wanunue. Wanataka samaki wawe kwenye ubora gani. Wanaridhika na bei unayowauzia.

**Jinsi Ya Kukuza Soko La Kambale**

Hakikisha samaki wako katika hali ya usafi na vyombo salama unapovua tayari kwa kupeleka sokoni. Samaki ni bidhaa inayoharibika kwa haraka, hivyo hakikisha unawapeleka sokoni mara tu baada ya kuwavua.

Hakikisha gharama za usafiri, utunzaji na uhifadhi, zinalipwa kutokana na bei ya soko. Kumbuka gharama za uhifadhi wa bidhaa inayoharibika haraka kama samaki ni kubwa, hivyo vua kwa awamu kulingana na mahitaji.

Unaweza kuongeza thamani ya samaki kwa kufanya mambo ya msingi yanayohitajika kwenye uandaaji wa samaki, kama vile kuparua na kutumbua.

Unaweza kuwasafisha, na pia kuwakaanga kulingana na soko husika. Kwa kuzingatia mambo hayo machache, mfugaji anaweza kufanya maamuzi sahihi kabla ya kuwekeza kwenye mradi wa ufugaji wa samaki.

Pia ni muhimu kuzingatia mahitaji muhimu ya ufugaji wa samaki, ili kuepuka gharama zisizo za lazima.

**Jinsi Ya Kutengeneza Chakula Cha Samaki**

Mfugaji anaweza kupunguza gaharama za kununua chakula kwa ajili ya samaki, kwa kutengeneza chakula mwenyewe kwa kutumia malighafi ulizo nazo katika eneo lako.

Tumia resheni rahisi ambayo itakupatia chakula cha kutosha na kwa gharama nafuu.

**Mahitaji Ya Chakula Cha Samaki**

Pumba ya mahindi sadolini 1. Pumba ya ngano au mpunga sadolini 1. Dagaa sadolini 1. Kilo moja ya soya. Robo kilo ya mashudu ya pamba au alizeti.

Jinsi Ya Kuandaa Chakula Cha Samaki

Changanya malighafi hizo kwa pamoja. Saga hadi zilainike. Kanda kama vile unga wa kutengenezea chapati. Weka kwenye mashine ya kusaga nyama au kutengenezea tambi. Anika kwenye jua la wastani.

Baada ya kukauka, vunja vunja kwenye vipande vidogo vidogo hasa kwa kuzingatia umri wa samaki unaokusudia kuwalisha.

Tumia lishe hiyo kwa samaki mara tatu kwa siku.



# Ukitaka kufuga kuku wa mayai fuata haya



NA MWANDISHI MAALUM

**Kuku wa mayai ni aina ya kuku wanaofugwa maalum kwa ajili ya uzalishaji wa mayai.**

Ili kufanikisha mradi wa kuku wa mayai, ni muhimu kufuata mbinu bora za ufugaji, kuanzia maandalizi ya banda, lishe, na huduma za afya.

Hapa chini ni mwongozo wa hatua kwa hatua wa kufuga kuku wa mayai kwa mafanikio.

**1. Faida za Kufuga Kuku wa Mayai**

Uzalishaji wa Muda Mrefu: Kuku wa mayai wana uwezo wa kutaga kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja. Soko Imara: Mayai yana soko kubwa na endelevu. Bidhaa Zenye Thamani: Mayai yana virutubisho muhimu, na mabaki ya kuku wanaweza kutumika kama nyama au mbolea.

**2. Kuandaa Banda la Kuku wa Mayai**

Banda bora ni muhimu kwa uzalishaji wa kuku wa mayai: Ukubwa wa Banda: Kuku mmoja anahitaji futi za mraba 1.5. Vifaa vya Kutagia: Weka vyombo vya kutagia vilivyofunikwa vizuri ili kuhakikisha usafi wa mayai.

Uingizaji wa Hewa: Banda liwe na madirisha ya kutosha kwa mzunguko wa hewa safi. Udhibiti wa Joto: Hakikisha banda lina vifaa vya kudhibiti joto, hasa wakati wa baridi.

**3. Chakula na Lishe ya Kuku wa Mayai**

Lishe bora ni muhimu kwa uzalishaji wa mayai yenye ubora:

Layer Mash: Tumia chakula cha kiwandani kilichoandaliwa maalum kwa kuku wa mayai.

Virutubisho vya Ziada: Ongeza madini ya calcium na phosphorus ili kuimarisha ganda la yai.

Vyakula vya Asili: Unaweza kuongeza mboga kama mchicha na majani ya maboga kwa kuku.

Maji Safi: Hakikisha maji safi yanapatikana muda wote.

**4. Huduma za Afya**

Kuku wa mayai wanahitaji huduma bora ya afya ili kuzuia magonjwa:

Chanjo Muhimu: Kama vile Newcastle na Infectious Bronchitis.

Udhibiti wa Vimelea: Tumia dawa za kuondoa minyoo na kuua viroboto.

Usafi wa Banda: Safisha mara kwa mara ili kuepusha magonjwa.

**5. Ratiba ya Mwanga**

Mwanga ni muhimu kwa kuku wa mayai ili kuhamasisha utagaji: Masaa 16 ya Mwanga: Hakikisha kuku wanapata mwanga wa kutosha kila siku.

Tumia Balbu: Tumia balbu za mwanga wa wastani ndani ya banda wakati wa usiku.

**6. Uvunaji wa Mayai**

Kusanya mayai mara mbili au tatu kwa siku ili kuepuka kupasuka. Safisha mayai kwa upole kwa kutumia maji masafi.

Hifadhi mayai mahali pakavu na penye ubaridi.

**7. Masoko ya Mayai**

Rejareja: Uza mayai moja kwa moja kwa wateja wa kawaida.

Wauzaji wa Jumla: Tafuta masoko ya jumla kama hoteli, migahawa, na maduka makubwa.

Mayai ya Mbegu: Unaweza kuuza mayai kwa wafugaji wanaohitaji kuku wa mbegu.

**8. Changamoto za Kufuga Kuku wa Mayai**

Gharama kubwa za chakula. Hatari ya magonjwa kama mdondo.

Kupungua kwa utagaji kuku wanapozeeka. Hata hivyo, changamoto hizi zinaweza kushughulikiwa kwa usimamizi bora, lishe sahihi, na huduma za afya.

**Hitimisho**

Kufuga kuku wa mayai ni mradi wenye faida ikiwa utafuata mbinu sahihi za ufugaji.

Uwekeze katika banda bora, lishe yenye virutubisho, na ufuate ratiba ya chanjo.

Kwa kujituma na kufuata mwongozo huu, unaweza kufanikisha mradi wako na kuongeza kipato kupitia uzalishaji wa mayai.



# Unataka kutoboa kwa kulima mpunga?



NA MWANDISHI WETU

**KILIMO cha mpunga ni miongoni mwa shughuli za kilimo zinazochangia kwa kiasi kikubwa chakula na uchumi duniani kote.**

Mpunga ni zao linalohitaji mali mengi uangalizi wa karibu, na utekelezaji wa kanuni bora ili kufanikisha mavuno mengi na yenye ubora.

**ZIFUATAZO NI KANUNI BORA ZA KILIMO CHA MPUNGA AMBAZO ZINAWEZA KUMSAIDIA MKULIMA KUFIKIA MALENGO YAKE YA UZALISHAJI.**

**1. Uchaguzi Sahihi wa Eneo**

Mpunga hustawi vizuri kwenye maeneo ya mabonde yenye maji mengi au maeneo yanayoweza kumwagiliwa kwa urahisi.

Hali ya hewa: Mpunga unahitaji hali ya hewa ya joto la wastani kati ya 20°C hadi 35°C. Joto chini ya 15°C linaweza kuathiri ukuaji wa mpunga.

Udongo: Mpunga hustawi vizuri kwenye udongo wa mfinyanzi ambao una uwezo wa kuhifadhi maji. Udongo wenye rutuba, wenye pH ya kati ya 5.5 hadi 7 ni bora zaidi kwa uzalishaji wa mpunga.

**2. Uchaguzi wa Mbegu Bora**

Uchaguzi wa mbegu ni hatua muhimu sana katika kilimo cha mpunga kwani mbegu bora zina uwezo wa kutoa mavuno mengi na yanayostahimili magonjwa na wadudu.

Mbegu za asili: Mbegu za kienyeji ambazo zimezoeleka katika eneo lako zinaweza kuwa na uwezo wa kuvumilia magonjwa ya eneo hilo.

Mbegu za kisasa (hybrid): Aina hizi zina sifa ya kutoa mavuno mengi zaidi, kukua haraka, na zinastahimili magonjwa mengi.

Kwa ekari moja, inashauriwa kutumia kiasi cha kilo 25 hadi 30 za mbegu.

**3. Maandalizi ya Shamba**

Maandalizi bora ya shamba yanawezesha mpunga kukua vizuri na kupata virutubisho muhimu kutoka kwenye udongo.

Kulima shamba: Shamba linapaswa kulimwa kwa kina ili kufyeka magugu na kuhakikisha udongo unakuwa laini na wenye hewa ya kutosha. Kwa kawaida, kulima kwa trekta ni bora zaidi, lakini pia unaweza kutumia jembe la mkono au ng'ombe.

Kusawazisha shamba: Kusawazisha shamba husaidia kuhakikisha maji yanasambaa vizuri kwenye eneo lote la shamba. Pia, inawezesha mimea ya mpunga kukua kwa usawa.

**4. Kuandaa Kitalu**

Mpunga unahitaji kuandaliwa kitalu kwanza kabla ya kupandikizwa kwenye shamba kuu.

Kitalu kinatayarishwa kwa uangalifu ili miche iweze kukua imara.

Kutengeneza kitalu: Kitalu kinapaswa kuwa eneo lenye udongo wenye rutuba na uwezo wa kutunza maji. Mbegu hupandwa kwa wingi kwenye kitalu na kumwagiliwa maji ya kutosha.

Kumwagilia miche: Miche ya mpunga inapaswa kumwagiliwa mara kwa mara na kuhakikisha kuwa inapata maji ya kutosha bila maji kupita kiasi.

Kupandikiza shambani: Baada ya siku 20 hadi 30, miche inakuwa tayari kupandikizwa shambani ikiwa na urefu wa sentimita 15 hadi 20.

**5. Kupandikiza Mpunga**

Kupandikiza mpunga ni hatua ya kuhamisha miche kutoka kitaluni kwenda kwenye shamba kuu.

Ni muhimu kufuata mbinu bora za kupandikiza ili kuepusha upotevu wa miche.

Umbali wa kupanda: Miche inapaswa kupandikizwa kwa umbali wa 20 cm x 20 cm kati ya mimea na mistari. Umbali huu unaruhusu mpunga kupata nafasi ya kutosha kwa ukuaji bora wa mizizi na kusaidia uingizaji wa hewa na mwanga.

Mbolea wakati wa kupandikiza: Ni muhimu kuweka mbolea ya asili kama samadi au mboji wakati wa kupandikiza ili kuongeza rutuba ya udongo.

**6. Umwagiliaji wa Maji**

Mpunga ni zao linalohitaji maji mengi ili kukua vizuri.

Hivyo, kumwagilia maji ni moja ya mambo muhimu katika kilimo cha mpunga.

Umwagiliaji wa mara kwa mara: Mpunga unahitaji umwagiliaji wa maji wa mara kwa mara kwa kuwa hautakiwi kukauka. Wakati wa kupandikiza, hakikisha kuwa shamba lina maji ya kutosha, kiasi cha sentimita 5 hadi 10 juu ya udongo.

Udhibiti wa maji: Baada ya miche kuota vizuri, ni muhimu kudhibiti kiwango cha maji na kuacha maji kupungua hadi sentimita 2 hadi 3 juu ya udongo. Hii husaidia mizizi ya mimea kukua vizuri bila kuathiriwa na maji mengi.

# TIWA SAVAGE ATETEA UMRI



LAGOS, Nigeria

**LEJENDARI wa Afrobeats, Tiwa Savage, amesema mashabiki wake wengi wanamuona hajui kuvaa viwalo vinavyokwenda na wakati.**

Hata hivyo, kwa mujibu wa bibiye huyo, hawezi kuvaa kama mabinti wa kisasa kutokana na umri wake mkubwa.

Kwa upande wake, Tiwa Savage alienda mbali zaidi na kusema kwa umri wake hawezi kuvaa kama akina Beyonce.

# ARJUN NDO' HIVYO TENA

NEW DELHI, India

**STAA wa filamu za Kihindi, Allu Arjun, anashikiliwa na polisi baada ya tukio la watu wawili kupoteza maisha wakiwa 'lokesheni'.**

Kwa mujibu wa ripoti, Arjun alikuwa kwenye maandalizi ya filamu yake ya 'Pushpa 2: The Rule' na aliyepoteza maisha ni mwanamke na mtoto wake wa kiume, huku watu kadhaa wakipata majeraha.

Ripoti zinaeleza kuwa tukio hilo lilisababishwa na maelfu ya mashabiki walio kuwa wamekusanyika nje ya ukumbi uliokuwa unatumika kwa maandalizi.



# DAVIDO MWANZO MWISHO

LAGOS, Nigeria

**MKALI wa Afrobeats, Davido, ameweka rekodi ya kuwa na wimbo uliofuatiliwa zaidi ndani ya wiki moja tangu uwekwe Spotify.**

Davido, ambaye jina lake halisi ni David Adeleke, anakuwa msanii wa kwanza wa Nigeria kufikisha idadi hiyo.

Ifahamike kuwa Davido ameingia kwenye historia kupitia wimbo wake wa 'Funds' na ameipita rekodi ya Wizkid.





# RASHFORD



## BASI TENA MAN UNITED

MANCHESTER, ENGLAND

STRAIKA wa Uingereza Marcus Rashford, ambaye amejiunga na klabu ya Aston Villa kwa mkopo, huenda asicheze tena Man United kwa vile uhusiano kati ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na timu hiyo ya Old Trafford umesambaratika.

## KLUIVERT KUTUA NEWCASTLE UTD

LONDON, England

TIMU ya Newcastle United inajiandaa kumsajili msahambuliaji wa Bournemouth na Uholanzi Justin Kluivert, 25, ikimkosa mshambuliaji wa Uswidi Alexander Isak, 25, msimu wa joto. (Sun)

Wakati huohuo, Newcastle na Tottenham huenda zikafufua nia ya kumsajili mlinzi wa Crystal Palace Marc Guehi, 24, msimu wa joto atakapoingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake, baada ya Spurs kukataliwa ofa mwishoni mwa dirisha la Januari.



## ARTETA AMUWANIA NICO

MADRID, Hispania

WINGA wa Athletic Bilbao wa Uhispania Nico Williams, 22, ni kipaumbele wa cha usajili wa mkufunzi wa Arsenal Mikel Arteta.

Kiungo wa Arsenal na timu ya taifa ya Italia Jorginho, 33, ametia saini makubaliano ya awali ya mkataba wa kujiunga na Flamengo ya Brazil msimu ujao wakati mkataba wake na The Gunners utakapokamilika.



## CONTE AMSIKITIKIA GARNACHO

MILAN, Italia

KOCHA wa Napoli Antonio Conte amesikitishwa na hatua ya klabu hiyo kutomsajili winga wa Manchester United na Argentina Alejandro Garnacho, 20, au mshambuliaji wa Ujerumani Karim Adeyemi, 23, kutoka Borussia Dortmund


Conte amesikitika baada ya kushindwa kukamilisha dili la kumchukua mmoja kati ya wachezaji hao baada ya baada ya kumuuza winga wa Georgia Khvicha Kvaratskhelia, 23, kwa Paris St-Germain.



## SIRI ZA NKUNKU HIZI HAPA

LONDON, England

KLABU za Manchester United na Bayern Munich zote zilimtaka mshambuliaji wa Ufaransa Christopher Nkunku mwezi Januari lakini zilisitisha mpango huo kwa sababu Chelsea iliongeza dau kwa mchezaji huyo.



Mjasiriamali spoti

MJASIRIAMALI FEBRUARI 5, 2025

Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# PACOME AWINDWA

## >>SIMBA YAMTAZAMA NJE NDANI, KAZI IPO

NA ASHA SEKEFU

MWAMBA mwenye kucheza na kutoa maelekezo ndani ya kikosi cha Yanga, Pacome Zouzoua ni pasua kichwa kutokana na uwezo wake kwenye kupiga pasi ndefu na fupi akiwa uwanjani.

Nyota huyo kwenye dirisha dogo ilikuwa inatajwa kuwa yupo kwenye rada za mabosi wa Simba kwa kuwa mkataba wake unagota mwisho inaelezwa kuwa mabosi wa Yanga walifanya mazungumzo naye kuhusu kuboresha mkataba wake akagoma.

Sasa, inaelezwa Simba ipo katika rada za kushusha jembe hilo Msimbazi na mipango kumnasa dirisha kubwa la usajili.

Habari ambazo gazeti hili linazo ni kwamba mipango yote ya Pacome kutua Simba inaenda freshi, na menejimenti yake imeshafanya mazungumzo na bosi kubwa, Mohamed Dewji jinsi ya dili hilo litakavyokwenda.

Lakini pia, inaelezwa ndoto ya Pacome kufika mbali kimataifa na sehemu anaona itakuwa ya kutimiza ndoto yake ni kwa Wekundu hao wa Msimbazi.


Mbali na hilo, lakini Pacome anaona Simba hawabanii kama mchezaji akipata dili la kupata timu nyingine nje ya Tanzania, anaweza kuuzwa bila milolongo mirefu ya kuachiwa.

Hivi karibuni Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally aliweka wazi kuwa wanamfuatilia mchezaji huyo kwa kuwa wanatambua mkataba wake unakaribia kuisha wakiona anafaa watahangaika naye.

"Kuna mchezaji ambaye yupo pale ambaye ni Pacome huyu tunamfuatilia tukiona anatufaa basi tutahangaika naye kwa kuwa tunajua kwamba mkataba wake unaisha." alisema .

Pacome ndani ya ligi amecheza jumla ya mechi 15 kati ya 16 akikosekana kwenye mchezo mmoja, akifunga mabao sita na kutoa pasi tatu za mabao.

Yanga kwa sasa ipo kwenye maandalizi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya KenGold ya Mbeya mchezo unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa KMC, Complex, keshokutwa.




# Samia Women Boxing Kiboko

NA MWANDISHI WETU

**MASHINDANO ya Samia Women Boxing Championship yamefikia tamati mwanzoni mwa wiki tangu yalipoanza Januari 31, mwaka huu katika fukwe za Kawe, jijini Dar es Salaam.**

Katika fainali hizo mapambano nane yamefanyika huku pambano moja pekee likishandikina kufanyika kwa mpinzani wa Konsolata Laiza ambaye ni Fatuma Yazidu kushindwa kupanda ulingoni.

Kwenye pambano la kwanza Veronika Thomas kutoka makao makuu JKT amemtandika Leylat Kwa 'points'.

Pambano la pili Latifa Said kutoka JKT ameshinda Sarafina Fusi wa timu ya Ngome kwa 'points'.

Wakati pambano la tatu Tatiana Ezekiel kutoka Gym ya Zugo amempiga Debora mwenda kutoka kwenye Gym ya Mzee Kinyogoli kwa 'points'.

Huku pambano la nne Vumilia Kalinga wa timu ya Ngome alimchakaza kwa 'points' Zawadi Amosi wa timu ya Makao Makuu JKT. Halima Vunjabei kutoka Maccoz Gym akapata ushindi wa 'TKO' dhidi ya Mariam Jonasi wa timu ya Balax kwenye raundi ya pili ya pambano la raundi tatu.

Pambano la sita Dolikas Daud kutoka gym ya Uwanja wa kivita ameibuka kidedea kwa kumchapa Zulafa Iddi wa Gym ya Zugo kwa 'points'. La saba Najima Isike wa timu ya Taifa ya ngumi alipata ushindi wa 'points' dhidi ya Joyce Saitabaru kutoka Polisi Arusha.

Huku pambano la nane Rachael Msingo kutoka Dodoma alimtandika Mariam Msabila kwa 'points' kutoka gym ya Mzee Kinyogoli.

Mashindano hayo yalianza mnamo Januari 31 mwaka huu na kufikia tamati juzi ambapo kwa siku zote tatu mapambano hayo yalifanyika kwa kuratibiwa na Shirikisho la Ngumi Tanzania (BFT).

